# Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu
**&**
# Mkataba wa Nyongeza (2006)
(Tafsiri isiyo rasmi)

**Umoja wa Mataifa (New York-)**

## Dibaji

**Walioridhia Mkataba huu, kwa**

(a) Kukumbuka kanuni zilizobainishwa ndani ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa ambao unatambua hadhi ya asili, thamani, usawa na haki zisizopokonyeka za watu wote ambao ni wa jamii ya binadamu kama uhuru wa msingi, haki na amani duniani;

(b) Kutambua kwamba Umoja wa Mataifa, katika Tamko la Dunia la Haki za Binadamu na Mikataba ya Kimataifa ya Haki za Binadamu, umetangaza na kukubali kwamba kila mmoja ana stahili kupata haki zote na uhuru kama zinavyoelezwa humo, bila tofauti ya aina yoyote;

(c) Kuthibitisha kwa msisitizo hali ya kuwahusu watu wote, kutogawanyika, kutegemeana, na kuhusiana kwa haki zote za binadamu na uhuru wa msingi na uhitaji wa watu wenye ulemavu kuhakikishiwa kunufaika kwao kikamilifu bila ubaguzi;

(d) Kukumbuka Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni, Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na za Kisiasa; Mkataba wa Kimataifa wa kuondosha aina zote za Ubaguzi wa Rangi; Mkataba wa Kimataifa wa Kukomesha aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake; Mkataba Dhidi ya Mateso na Adhabu au Matendo Mengine ya Kikatili, yasiyo ya Kibinadamu au ya Kiudhalilishaji; Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto, na Mkataba wa Kimataifa wa Ulinzi wa Haki za Wafanyakazi wote Wahamiaji na Familia zao;

e) Kutambua kuwa ulemavu ni dhana inayobadilika na kwamba ulemavu hutokea kutokana na mchangamano baina ya watu wenye ulemavu na mitizamo na vikwazo vya kimazingira, ambavyo huzuia ushiriki wao kamili na unaofaa kwa jamii katika hali iliyo sawa na wengine;

(f) Kutambua umuhimu wa kanuni na miongozo ya kisera iliyomo ndani ya Mpango Kazi wa Dunia kuhusu Watu wenye Ulemavu na kwenye Kanuni Sanifu za kuweka Usawa wa Fursa kwa Watu wenye Ulemavu katika kushawishi uendelezaji, utungaji na utathmini wa sera, mipango, programu, na hatua mbali mbali katika ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa ili kutoa fursa sawa kwa watu wenye ulemavu,

(g) Kutilia mkazo umuhimu wa kujumuisha masuala ya ulemavu kama sehemu ya lazima ya mikakati inayohusiana na maendeleo endelevu,

(h) Kutambua pia kuwa ubaguzi dhidi ya mtu yeyote kwa msingi wa ulemavu ni uvunjaji wa hadhi ya asili na thamani ya nafsi ya binadamu;

(i) Kutambua zaidi uanuwai miongoni mwa watu wenye ulemavu;

(j) Kutambua haja ya kukuza na kulinda haki za binadamu za watu wote wenye ulemavu, wakiwemo wale wanaohitaji msaada maalum wa ziada;

(k) Kuguswa kwamba, licha ya kuwepo kwa mikataba na kuchukuliwa kwa hatua mbali mbali, bado watu wenye ulemavu wameendelea kukabiliwa na vikwazo katika ushiriki wao kama wanajamii walio sawa na wengine na haki zao za kibinadamu huvunjwa duniani kote,

(l) Kutambua umuhimu wa ushirikiano wa kimataifa katika kuboresha hali za maisha ya watu wenye ulemavu katika kila nchi, hususan zile zinazoendelea,

(m) Kutambua thamani ya mchango unaotolewa na unaoweza kutolewa na watu wenye ulemavu katika maendeleo ya jumla ya binadamu na uanuwai uliopo katika jumuiya zao, na kwamba kwa

kuhamasisha kunufaika kikamilifu na haki zao za binadamu, Uhuru wa msingi, na ushiriki wao kikamilifu, kutawawezesha kujihisi kuwa sehemu ya jamii na kwa kiwango kikubwa kuelekea kwenye hatua za maendeleo ya kibinadamu, kijamii na kiuchumi na katika kutokomeza umaskini;

(n) Kutambua umuhimu wa watu wenye ulemavu kwa kila mmoja kujiamulia mambo mwenyewe binafsi na kujitegemea ikiwa ni pamoja na uhuru wa kuchagua mwenyewe yale anayoyataka;

(o) Kuzingatia kwamba watu wenye ulemavu wanapaswa kupata fursa ya kushirikishwa kikamilifu katika michakato ya kufanya maamuzi yahusuyo sera na mipango mingine, ikiwa ni pamoja na ile inayowahusu wao moja kwa moja;

(p) Kuguswa na hali mgumu wanazowakabili watu wenye ulemavu ambao wamekuwa waathirika wa aina mbali mbali au zilizokithiri za ubaguzi kwa misingi ya koo, rangi, jinsi, lugha, dini, siasa au itikadi nyinginezo, utaifa, uzawa au sehemu atokayo mhusika, ukwasi, umri au hali nyinginezo;

(q) Kutambua kuwa wanawake na wasichana wenye ulemavu wanapokuwa nyumbani au nje ya nyumbani kila wakati wako katika hatari kubwa zaidi ya kufanyiwa ukatili, kujeruhiwa au kudhalilishwa, kutelekezwa au kuhudumiwa kizembe, kutendewa vibaya au kudhulumiwa;

(r) Kutambua kuwa watoto wenye ulemavu wanapaswa kunufaika kikamilifu na haki zote za binadamu na uhuru wa msingi kwa kuzingatia usawa na watoto wengine, na kwa kukumbuka wajibu wa jinsi hiyo uliochukuliwa na nchi wanachama wa Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto;

(s) Kusisitiza hitaji la kujumuisha mtazamo wa jinsia katika jitihada zote za kuendeleza unufaikaji kamili wa haki za binadamu na haki za msingi kwa watu wenye ulemavu;

(t) Kuonyesha ukweli kwamba watu wengi wenye ulemavu huishi katika hali ya umasikini, na kwa maana hiyo, kutambua uhitaji mahususi wa kushughulikia athari mbaya za umaskini kwa watu wenye ulemavu;

(u) Kutafakari kwamba hali ya amani na usalama unaozingatia kuheshimu kikamilifu madhumuni na kanuni zilizoainishwa kwenye Hati ya Umoja wa Mataifa na uzingatiaji wa mikataba mbalimbali ya haki za binadamu iliyopo kuwa ni ya lazima katika kuwalinda watu wenye ulemavu, hususan, wakati wa mapambano ya silaha na kuvamiwa kimabavu na wageni;

(v) Kutambua umuhimu wa kuyafikia mazingira yanayoonekana, ya kijamii, ya kiuchumi na yale ya kiutamaduni, kuifikia miundombinu ya kiafya na kielimu, na kuweza kupata habari na mawasiliano, ili kuwawezesha watu wenye ulemavu kunufaika kikamilifu na haki zote za binadamu na Uhuru wa misingi;

(w) Kutambua kuwa kila mmoja, anao wajibu kwa wenzake na kwa jamii anamotoka anakabiliwa na jukumu la kujibiidiisha kwa ajili ya kuendeleza na kutekeleza uzingatiaji wa haki zinazotambuliwa kwenye Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu;

(x) Kusadiki kuwa familia ni kundi la kiasili, la msingi katika jamii na lenye haki ya kulindwa na jamii na dola, na kwamba watu wenye ulemavu na familia zao wanapaswa kupata ulinzi na msaada unaohitajika ili kuziwezesha (familia) kuchangia kwa ukamilifu na kwa usawa katika unufaukaji na haki za watu wenye ulemavu;

(y) Kusadiki kuwa Mkataba wa Kimataifa wenye upeo mpana na uliotengemaa wa kuendeleza na kulinda haki na hadhi ya watu wenye ulemavu utatoa mchango wa maana katika kurekebisha mapungufu yanayowakabili watu wenye ulemavu na kupanua ushiriki wao wa fursa sawa katika nyanja za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni, katika nchi zote zinazoendelea na zilizoendelea,

Wamekubaliana kama ifuatavyo:

## Ibara ya 1
## Azma

Azma ya Mkataba huu ni kuendeleza, kulinda na kuhakikisha upatikanaji mkamilifu na sawa wa haki zote za binadamu na uhuru wa asili kwa watu wote wenye ulemavu, na kukuza uheshimikaji wa hadhi yao ya asili.

Watu wenye ulemavu ni pamoja na wale wenye udhoofu wa muda mrefu wa maumbile, akili au fahamu ambao ukichangamana na vikwazo mbalimbali, vinaweza kuzuia ushiriki wao kikamilifu na kimanufaa katika jamii kwa misingi ya usawa na watu wengine.

## Ibara ya 2
## Fasili

Kwa madhumuni ya Mkataba huu:

**"Mawasiliano**"-Ni neno lenye kujumuisha lugha mbalimbali, maonyesho ya matini, maandishi ya nukta nundu, lugha ya kupapasa, maandishi yenye herufi nene, vyombo mbalimbali vya habari vinavyopatikana, hali kadhalika na maandishi, sauti, lugha nyepesi, ving'amuzi vya vitendo, teknolojia za kukuza mawimbi ya sauti na namna, njia na mitindo mbadala ya kimawasiliano, ikijumuisha upatikanaji wa taarifa na teknolojia ya mawasiliano.

**"Lugha"**- Ni neno linalojumuisha lugha ya mazungumzo na lugha ya alama na aina nyingine za lugha zisizo za matamshi.

**"Ubaguzi kwa misingi ya ulemavu"**-Ni neno linalomaanisha kutofautishwa kokote, kutengwa au kuzuiwa kwa  kwa sababu ya ulemavu ambako kuna azma ya kudhoofisha au kubatilisha utambulisho, ufurahiaji

au utekelezwaji wa haki zote za kibinadamu na uhuru wa asili kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, kiraia au eneo lolote lile kwa misingi ya usawa na watu wengine. Ubaguzi ni pamoja na aina zote za ubaguzi, ikijumuisha na kunyimwa marekebisho stahili.

**"Marekebisho stahili"**-Ni neno linalomaanisha mabadilisho na marekebisho ya lazima na yafaayo bila kusababisha taabu isiyowiana au isiyovumilika, pale yanapohitajika kutokana na hali fulani, ili kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanafurahia au kutumia haki zote za binadamu na uhuru wa msingi kwa kiwango sawa na wengine.

**"Usanifu kwa ajili ya wote"-**Ni neno linalomaanisha ubunifu wa bidhaa, mazingira, mipango na utoaji huduma unaoweza kutumiwa na watu wote, kwa kiasi kikubwa kadri inavyowezekana, bila ya kuwepo haja ya kufanya marekebisho au matengenezo maalum. "Usanifu kwa ajili ya wote" hauondoi umuhimu wa kuwepo kwa nyenzo saidizi kwa ajili ya makundi maalum ya watu wenye ulemavu pale ambapo zinahitajika.

## Ibara ya 3
## Kanuni za Jumla:

Kanuni za a jumla za Mkataba huu zitakuwa ni:

(a)Kuheshimu hadhi ya asili, uhuru wa mtu binafsi ikiwa ni

pamoja na uhuru wa kufanya maamuzi yake mwenyewe, na kujitegemea kwa watu;

(b) Kutokubaguwa;
(c) Ushiriki kamili na wa maana na ujumuishwaji katika jamii;

(d)Kuheshimu tofauti na kuwakubali watu wenye ulemavu kuwa ni sehemu ya tofauti miongoni mwa binadamu na ubinadamu

(e) Usawa wa fursa;

(f) Ufikikaji;

(g) Usawa kati ya wanaume na wanawake;

(h)Kuheshimu uwezo wa watoto wenye ulemavu unaokua na kuheshimu haki za watoto wenye ulemavu na kuhifadhi utambulisho wao.

## Ibara ya 4
## Wajibu wa Jumla

1. Nchi Wanachama zinakubali kuhakikisha na kuendeleza upatikanaji kamilifu wa haki zote za binadamu na uhuru wa msingi kwa watu wote wenye ulemavu bila ubaguzi wa namna yoyote ile kwa misingi ya ulemavu. Ili kufikia azma hii, Nchi Wanachama zinakubali:

(a) Kuchukua hatua zote zinazohitajika za kutunga sheria, kiutawala na nyinginezo katika kutekeleza haki zilizotambuliwa ndani ya Mkataba huu;

(b) Zitachukua hatua zote zinazohitajika, zikiwemo za kisheria, kurekebisha au kufuta sheria zilizopo, kanuni, mila na desturi ambazo zinaendekeza ubaguzi dhidi ya watu wenye ulemavu;

(c) Zitazingatia ulinzi na uendelezaji wa haki za binadamu kwa watu wenye ulemavu katika sera zote na mipango yote;

(d) Zitajizuia kujiingiza katika jambo lolote lile linaloenda kinyume na Mkataba huu na kuhakikisha kuwa mamlaka na taasisi za umma zinafanya kazi zao kwa kuzingatia Mkataba huu;

(e) Zitachukua hatua zote zinazofaa ili kuondoa ubaguzi wa aina yoyote unaoweza kufanywa kwa misingi ya ulemavu na mtu yoyote, jumuiya au kampuni binafsi;

(f) Zitafanya au kuendeleza tafiti na maendeleo ya bidhaa, huduma, vifaa na nyenzo zilizosanifiwa kwa ajili ya wote kwa mujibu wa ibara ya 2 ya Mkataba huu, ambavyo vitahitaji marekebisho madogo kadri invyowezekana na kwa gharama nafuu ili kukidhi mahitaji maalum ya mtu mwenye ulemavu, kuhimiza upatikanaji na matumizi yake, na kuhimiza usanifu kwa ajili ya wote wakati wa kuendeleza viwango na miongozo.

(g) Zitafanya au kuendeleza tafiti, na kutengeneza au kukuza upatikanaji na matumizi ya teknolojia mpya, ikiwa ni pamoja na teknolojia ya habari na mawasiliano, zana za ujongeaji, nyenzo na teknolojia saidizi, zinazowafaa watu wenye ulemavu, kwa kuzipa kipaumbele teknolojia zenye gharama nafuu;

(h) Zitawajibika kutoa habari kwa watu wenye ulemavu juu ya upatikanaji wa nyenzo za kujimudu kujongea, nyenzo na teknolojia saidizi, ikijumuisha teknolojia mpya, pamoja na namna nyingine za usaidizi, huduma za usaidizi na vifaa;

(i) Zitakuza mafunzo ya wataalam na watumishi wanaoshughulika na watu wenye ulemavu juu ya haki zinazotambuliwa kwenye Mkataba huu ili kuboresha utoaji misaada na huduma zinazohakikishwa na haki hizo;

2. Kuhusu haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni, kila nchi iliyoridhia Mkataba huu itachukua hatua za kiwango cha juu kwa kadri rasilimali zake zinavyoruhusu, na pale inapobidi, kufanya hivyo katika mfumo wa ushirikiano wa kimataifa, ili hatua kwa hatua kufanikisha upatikanaji wa haki hizi kikamilifu, bila kuathiri wajibu uliopo ndani ya Mkataba huu bila kupuuzia utekelezaji wa majukumu yaliyoainishwa na Mkataba huu ambayo yanaanza kutumika mara moja kwa mujubu wa sheria za kimataifa.

3. Katika mchakato wa kutunga na kutekeleza sheria na sera za kutekeleza Mkataba huu, na katika michakato mingine ya kufanya maamuzi yanayohusu watu wenye ulemavu, waliouridhia Mkataba huu watashauriana kwa karibu na kuwashirikisha watu wenye ulemavu, ikiwa ni pamoja na watoto wenye ulemavu, kupitia jumuiya zinazowawakilisha.

4. Hapana jambo lolote ndani ya Mkataba huu litakaloathiri ibara yoyote ambayo inachangia zaidi katika kufikia upatikanaji wa haki za watu wenye ulemavu na ambayo imo katika sheria za waliouridhia Mkataba huu au Sheria ya Kimataifa inayotumika katika nchi hiyo. Hapatakuwepo vizuizi au kudharauliwa kwa haki zozote za binadamu na misingi ya uhuru ilizopo kwa mujibu wa sheria, mikataba ya kimataifa au desturi katika nchi yoyote ile iliyoridhia Mkataba kwa kisingizio kwamba Mkataba huu hautambui haki au uhuru huo au kwamba zinatambuliwa kwa kiwango cha chini.

5. Masharti ya Mkataba huu yatatumika katika maeneo yote ya nchi zenye mfumo wa shirikisho bila ya kuwepo mipaka au baadhi ya vipengele kuachwa.

## Ibara ya 5
## Usawa na kutokubagua

1. Waliouridhia Mkataba huu wanatambua kwamba watu wote ni sawa mbele na chini ya sheria na wanastahili kulindwa na kunufaishwa na sheria kwa usawa bila ubaguzi wowote.

2. Waliouridhia Mkataba huu watapiga marufuku aina zote za ubaguzi kwa misingi ya ulemavu na kubeba dhamana ya kuhakikisha kwamba, watu wenye ulemavu wanapewa ulinzi sawa na imara wa kisheria dhidi ya ubaguzi katika hali yoyote ile.

3. Ili kukuza usawa na kuondoa ubaguzi, waliouridhia Mkataba huu watachukua hatua zinazohitajika ili kuhakikisha kuwa marekebisho yanayostahili yanafanyika.

4. Hatua mahsusi ambazo ni za lazima katika kuharakisha au kufanikisha kwa vitendo usawa kwa watu wenye ulemavu, hazitochukuliwa kuwa ni ubaguzi chini ya masharti ya Mkataba huu.

## Ibara ya 6
## Wanawake wenye ulemavu

1. Waliouriudhia Mkataba huu wanatambua kuwa wanawake na wasichana wenye ulemavu wanakabiliwa na aina nyingi za ubaguzi, na kwa maana hiyo, zitachukua hatua ili kuhakikisha kuwa wananufaika kikamilifu na haki zote za binadamu na uhuru wa msingi.

2. Nchi Wanachama zitachukua hatua zote zinazofaa kuhakikisha maendeleo kamili, uendelezaji na uwezeshaji wa wanawake, kwa madhumuni ya kuhakikisha kwamba wanapata na kufurahia haki za binadamu na uhuru wa asili zilizoorodheshwa ndani ya Mkataba huu.

## Ibara ya 7
## Watoto wenye ulemavu

1. Waliouridhia Mkataba huu watachukua hatua zote za lazima katika kuhakikisha kwamba watoto wenye ulemavu wananufaika kikamilifu na haki zote za binadamu na uhuru wa msingi kwa kiwango sawa na watoto wengine.

2. Katika matendo yote yanayowahusu watoto wenye ulemavu, maslahi bora ya mtoto ndiyo yatakayozingatiwa.

3. Waliouridhia Mkataba huu watahakikisha kwamba watoto wenye ulemavu wanayo haki ya kutoa maoni yao kwa uhuru juu ya mambo yote yanayowahusu, mawazo yao yakipewa uzito unaostahiki kwa mujibu wa umri na upevu wao, kwa misingi sawa na watoto wengine, na wapatiwe visaidizi kwa kuzingatia aina ya ulemavu na umri wao ili kuipata haki hiyo.

## Ibara ya 8
## Kukuza Ufahamu

1. Waliouridhia Mkataba huu wamekubali kuchukua hatua za haraka, madhubuti na zinazofaa katika:

(a) Kukuza ufahamu katika jamii yote, ikiwemo ndani ya familia kuhusu watu wenye ulemavu, na kuendeleza heshima, haki na hadhi ya watu wenye ulemavu;

(b) Kupambana dhidi ya mazoea yaliyo ndani ya jamii, dharau, kinyongo na mienendo yenye madhara dhidi ya watu wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na ile yenye kuegemea jinsi na umri katika nyanja zote za maisha.

(c) Kuendeleza ufahamu kuhusu uwezo na michango ya watu wenye ulemavu.

2. Hatua za kufikia lengo hili ni pamoja na:

a) Kuanzisha na kuendeleza kampeni imara za ufahamu wa umma zinazolenga:

(i) Kuhakikisha haki za watu wenye ulemavu zinatambulika;

(ii) Kuendeleza elimu ya mapokeo ya haki za watu wenye ulemavu;

(iii) Kukuza utambuzi wa ujuzi, stahili na uwezo wa watu wenye ulemavu na mchango wao mahali pa kazi na katika soko la ajira.

(b) Kuendeleza katika ngazi zote za mfumo wa elimu, kadhalika miongoni mwa watoto wote tokea wakiwa na umri mdogo, tabia ya kuheshimu haki za watu wenye ulemavu;

(c) Kuvihimiza vyombo vyote vya habari kutangaza taswira ya watu wenye ulemavu kwa njia zinazokubaliana na makusudio ya Mkataba huu;

(d) Kuhamasisha uwepo wa programu za utambuzi kuwahusu watu wenye ulemavu na haki zao;

## Ibara ya 9
## Ufikikaji na upatikanaji

1. Katika kuwawezesha watu wenye ulemavu waishi kwa kujitegemea na kushiriki kikamilifu katika nyanja zote za maisha, waliouridhia Mkataba huu watachukua hatua zinazofaa ili kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu, sawa na watu wengine wanafika kwenye mazingira yaliyosanifiwa, mfumo wa usafiri, habari na mawasiliano ikiwa ni pamoja na mifumo na teknolojia ya habari, vifaa na huduma nyinginezo zilizo wazi na zitolewazo kwa umma mijini na vijijini. Pamoja na mambo mengine, hatua hizi, zitajumuisha uainishaji na uondoshaji wa mikingamo dhidi ya ufikikaji na utumikaji wa :

(a) Majengo, barabara, usafiri na vifaa vingine nje na ndani ya shule, majengo ya umma miundombinu ya afya na mahali pa kazi;

(b) Habari, mawasiliano na huduma nyingine ikijumuisha huduma za kielektoniki na zile za dharura;

2. Waliouridhia Mkataba huu pia watachukua hatua zinazofaa ili:

(a) Kuendeleza, kueneza na kufuatilia utekelezaji wa viwango vya kawaida na miongozo kuhusu upatikanaji wa huduma kwa ajili umma;

(b) Kuhakikisha kuwa taasisi zote binafsi zinazotoa vifaa na huduma kwa ajili ya umma zinazingatia kuwa huduma zao zinawafikia watu wenye ulemavu;

(c) Kutoa mafunzo kwa wadau juu ya matatizo ya watu wenye ulemavu katika upatikanaji wa huduma;

(d) Kuweka ndani ya majengo na sehemu nyingine zinazohudumia umma alama kwa maandishi ya Nukta Nundu na kwa njia nyingine zinazosomeka na kueleweka kirahisi;

(e) Kutoa visaidizi halisi na wasaidizi, ikiwa ni pamoja na waongozaji, wasomaji na wakalimani mabingwa wa lugha ya alama ili kuwawezesha watu wenye ulemavu kuyafikia na kuyatumia majengo na huduma nyinginezo kwa ajili ya umma;

(f) Kuhamasisha njia nyingine sadifu za usaidizi ili kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanapata habari/taarifa;

(g) Kuhamasisha upatikanaji wa aina mpya za teknolojia na mifumo ya habari na mawasiliano, ikiwa ni pamoja na intaneti kwa ajili ya watu wenye ulemavu

(h) Kuhamasisha usanifu, uendelezaji, uzalishaji na usambazaji wa teknolojia na mifumo ya habari na mawasiliano ili zipatikane kwa gharama nafuu.

## Ibara ya 10
## Haki ya Kuishi

Waliouridhia Mkataba huu wanasisitiza kuwa kila binadamu anayo haki ya asili ya kuishi na zitachukua hatua za makusudi ili kuhakikisha kwamba haki hiyo inafurahiwa kwa ukamilifu na watu wenye ulemavu kwa misingi iliyo sawa na watu wengine.

## Ibara ya 11
## Hali za hatari na dharura

Waliouridhia Mkataba huu watachukua hatua za makusudi, kulingana na wajibu unaobainishwa chini ya Sheria ya Kimataifa, ikijumuisha Sheria ya Kimataifa ya Misaada ya Kibinadamu na Sheria ya Kimataifa ya Haki za Binadamu katika kuhakikisha ulinzi na usalama kwa watu wenye ulemavu

wakati wa hali ya hatari, ikiwa ni pamoja na mazingira ya mapigano ya silaha, dharura za kibinadamu na matukio ya majanga ya asili.

## Ibara ya 12
## Kutambuliwa kwa usawa mbele ya Sheria

1. Waliouridhia Mkataba huu wanasisitiza kwamba watu wenye ulemavu wana haki ya kutambuliwa mahali popote kama watu mbele ya sheria.

2. Waliouridhia Mkataba huu watatambua kwamba watu wenye ulemavu wanafurahia kuwa na uwezo wa kisheria kwa misingi ya usawa na watu wengine katika nyanja zote za kimaisha.

3. Waliouridhia Mkataba huu watachukua hatua zinazofaa ili kuwawezesha watu wenye ulemavu kupata msaada wa kisheria watakaouhitaji katika kutekeleza uhalali wao wa kisheria.

4. Waliouridhia Mkataba huu watahakikisha kwamba hatua zote zinazohusiana na uhalali wa kutenda kisheria zina kinga zinazofaa kuzuia matumizi mabaya kwa mujibu wa sheria ya Kimataifa ya Haki za Binadamu. Kinga za aina hii zitahakikisha kuwa hatua zinazohusiana na uhalali wa kutenda kisheria zinaheshimu haki, utashi na upendeleo wa mtu, hazina mgongano wa kimaslahi na ushawishi usiostahili, zinawiana na kuendana na hali ya mhusika, zinatumika katika muda mfupi kadri inavyowezekana na zinapitiwa mara kwa mara na mamlaka zinazojitegemea, zenye uwezo na adili au chombo cha kimahakama. Kinga hizo zitawiana na kiwango ambacho hatua hizo huathiri haki na maslahi ya mhusika.

5. Kwa mujibu wa masharti ya ibara hii, Waliouridhia Mkataba huu watachukua hatua zote zinazofaa na madhubuti katika kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wana haki sawa ya kumiliki au kurithi mali, kusimamia mambo yao ya kifedha na haki sawa ya kupata mikopo ya kibenki, uwekaji rehani na njia nyinginezo za mikopo, na zitahakikisha kwamba watu wenye ulemavu hawanyang’anywi mali zao kiholela.

**Ibara ya 13**
**Upatikanaji wa haki:**

1. Waliouridhia Mkataba watahakikisha upatikanaji wa haki stahiki kwa watu wenye ulemavu katika misingi ya usawa na watu wengine, ikijumuisha marekebesho ya vipengele vya utaratibu wa kiuendeshaji yanayozingatia umri, ili kufanikisha jukumu lao kama washiriki wa moja kwa moja au wasiyo wa moja kwa moja na kuwa mashahidi katika mienendo yote ya kesi na katika hatua za upelelezi na hatua nyingine za awali.

2. Ili kusaidia kuhakikisha upatikanaji wa haki kwa watu wenye ulemavu, Waliouridhia Mkataba huu watatoa mafunzo kwa wale wanofanya kazi katika tasnia ya utoaji haki wakiwemo polisi na wafanyakazi wa magereza.

**Ibara ya 14**
**Uhuru na Usalama wa mtu**

1. Waliouridhia Mkataba watahakikisha kuwa, katika misingi ya usawa na wengine, wale wenye ulemavu nao:

(a) Wanafurahia haki ya uhuru na usalama wa mtu;

(b) Hawapokonywi uhuru wao kinyume cha sheria au kiholela, na kwamba ikibidi kupokonywa uhuru wao, basi iwe ni kwa mujibu wa sheria, na kwamba kuwa na ulemavu kwa namna yoyote ile hakutohalalisha kupokonywa kwa uhuru.

2. Waliouridhia Mkataba huu watahakikisha kwamba, ikiwa watu wenye ulemavu kwa njia yoyote ile wamepokonywa uhuru wao, basi kwa msingi sawa na wengine, wana haki ya kuhakikishiwa uhuru wao kwa mujibu wa sheria za kimataifa za haki za binadamu na watatendewa kwa mujibu wa

malengo na misingi ya Mkataba huu, ikijumuisha na kipengele cha marekebisho yanayostahili.

**Ibara ya 15**
**Uhuru wa kutoteswa, au kudhalilishwa**

1. Hapana mtu atakayewekwa katika hali ya mateso au udhalimu, kutendewa au kuadhibiwa kinyume cha ubinadamu, kiudhalilishaji au kikatili. Kwa namna yoyote ile, hakuna mtu atakayefanyiwa majaribio ya kitabibu au kisayansi bila yeye kuridhia kwa uhuru.

2. Nchi Wanachama zitachukua hatua madhubuti za kisheria, kiutawala, kijamii, kielimu na hatua nyingine ili kuwalinda watu wenye ulemavu katika misingi ya usawa na watu wengine, ili wasiteswe, wasifanyiwe udhalimu, kudhalilishwa kinyume cha ubinadamu.

**Ibara ya 16**
**Kutonyonywa, kutofanyiwa ukatili na kutodhalilishwa**

1. Waliouridhia Mkataba huu watachukua hatua stahiki za kisheria, kiutawala, kijamii, kielimu na hatua nyingine ili kuwalinda watu wenye ulemavu nje na ndani ya familia zao dhidi ya vitendo vya kinyonyaji, kikatili na kidhalilishaji, ikiwa ni pamoja na upendeleo wa kijinsia.

2. Waliouridhia Mkataba huu pia watachukua hatua madhubuti ili kuzuia aina zote za unyonyaji, ukatili na udhalilishaji kwa kuhakikisha pamoja na mambo megine kuwepo kwa mifumo stahiki ya usaidizi inayozingatia jinsia na makundi rika ya watu wenye ulemavu, familia na walezi wao, ikijumuisha utoaji habari na elimu kuhusu mbinu za uzuiaji, kutambua na kuyatolea taarifa matendo ya kinyonyaji, kikatili na kidhalilishaji. Waliouridhia Mkataba huu watahakikisha kwamba huduma za kinga zinatilia maanani unyeti wa masuala ya umri, jinsia, na ulemavu.

3. Ili kuzuia aina zozote za kinyonyaji, kikatili, na kidhalilishaji, Waliouridhia Mkataba huu, watahakikisha kwamba nyenzo na mipango

ambayo inalenga kuwahudumia watu wenye ulemavu, inasimamiwa kimadhubuti na mamlaka zilizo huru.

4. Waliouridhia Mkataba huu, watachukua hatua madhubuti kuendeleza watu wenye ulemavu walioathiriwa kwa namna yoyote ile kutokana na kunyonywa,, kufanyiwa ukatili au kudhalilishwa, kwa kuwapatia ahueni kimwili, kiakili na kisaikolojia kwa njia ya kuwatengemaza na kuwarejesha kwenye jamii na hata kwa njia ya huduma za kinga. Ahueni hiyo na urejeshaji katika hali ya kawaida utafanyika katika mazingira yatakayoimarisha afya, ustawi, heshima, hadhi na uhuru wa mtu na utazingatia mahitaji ya kijinsia na ya makundi rika.

5. Waliouridhia Mkataba huu watatunga sheria na sera madhubuti, ikijumuisha sheria na sera zenye kuwalenga wanawake na watoto ili kuhakikisha matukio ya kinyonyaji, kikatili na kidhalilishaji dhidi ya watu wenye ulemavu yanabainishwa, yanafanyiwa upelelezi na, inapobidi, kuyafungulia mashtaka.

## Ibara ya 17
## Kuheshimu tofauti za kimaumbile

Kila mtu mwenye ulemavu anayo haki ya kuheshimiwa kwa ukamilifu wake kimwili na kiakili kwa misingi ya usawa na watu wengine.

## Ibara ya 18
## Uhuru wa mtu kwenda atakapo na kuwa na utaifa

1. Waliouridhia Mkataba huu wanatambua haki za watu wenye ulemavu za kuwa huru kwenda popote watakapo, uhuru wa kuchagua makazi yao na utaifa kwa misingi iliyo sawa na watu wengine, ikijumuisha kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu:

(a) Wanayo haki ya kapata na kubadili utaifa na kutopokonywa utaifa wao kiholela au kwa misingi ya ulemavu wao;

(b) Hawanyimwi, kwa misingi ya ulemavu walio nao, uwezo wa kupata, kumiliki na kutumia hati za utaifa wao au hati nyingine za utambulisho, au kutumia michakatao stahiki kama vile taratibu za uhamiaji, kwa kadri zinavyoweza kuhitajika ili kuwawezesha kutumia haki yao ya uhuru wa kwenda watakapo.

(c) Wapo huru kuihama nchi yoyote ile, hii ikiwa ni pamoja na nchi yao ya asili;

(d) Hawanyimwi, kiholela au kwa msingi wa ulemavu walio nao, haki ya kuingia/kurudi kwenye nchi yao ya asili .

2. Watoto wenye ulemavu watasajiliwa mara baada ya kuzaliwa na watakuwa na haki, toka wanapozaliwa ya kupewa jina, haki ya kupata utaifa na kwa kadri itavyowezekana, haki ya kuwatambua na kulelewa na wazazi wao.

## Ibara ya 19
## Kuishi kwa kujitegemea na Kujumuishwa katika jamii

Waliouridhia Mkataba wanatambua haki sawa kwa watu wote wenye ulemavu kuishi katika jamii, wakiwa na maamuzi sawa na watu wengine, na zitachukua hatua za makusudi katika kuwawezesha kufurahia haki hii kikamilifu, kujumuishwa na kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii, ikiwa ni pamoja na na kuhakikisha kwamba:

(a) Watu wenye ulemavu wanapata fursa ya kuchagua makazi yao, wataishi wapi na wataishi na nani kwa misingi iliyo sawa na watu wengine na hawalazimiki kuishi katika mfumo maalum ulioandaliwa;

(b) Watu wenye ulemavu wanapata huduma za aina mbalimbali nyumbani, kwenye eneo wanapoishi na huduma nyinginezo za kijamii zikijumuisha misaada binafsi ambayo ni ya lazima katika kuwawezesha kuishi na kujumuika kwenye jamii, na kuishi bila kutengwa au kubaguliwa na jamii inayowazunguka;

(c) Huduma za kijamii na miundombinu kwa ajili ya umma, inapatikana kwa watu wenye ulemavu kwa misingi ya usawa na inaendana na mahitaji yao.

## Ibara ya 20
## Matembezi binafsi

Waliouridhia Mkataba huu watachukua hatua madhubuti za kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanajitegemea kwa kadri inavyowezekana katika kumudu kutembea ikiwa ni pamoja na:

(a) Kumwezesha mtu binafsi mwenye ulemavu kutembea kwa namna na wakati anaotaka mwenyewe na kwa gharama atakayoimudu;

(b) Kuwawezesha watu wenye ulemavu kupata nyenzo bora za kujimudu, vifaa na teknolojia saidizi na aina nyingine ya usaidizi wa viumbe hai (wanadamu na wanyama) na vijumbe, ikijumuisha kuwezesha upatikanaji wake kwa gharama watakayoimudu;

(c) Kutoa mafunzo ya stadi za kutembea kwa watu wenye ulemavu na kwa watalaam wanaofanya kazi na watu wenye ulemavu;

(d) Kuzihimiza asasi zinazotengeneza nyenzo za kutembelea, vifaa na teknolojia saidizi kuzingatia vipengele vyote vya watu wenye ulemavu kumudu kutembea.

## Ibara ya 21
## Uhuru wa kujieleza, kutoa maoni na kupata habari

Waliouridhia Mkataba huu watachukua hatua zinazofaa katika kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanatumia haki ya uhuru wa kujieleza na kutoa maoni, ikijumuisha uhuru wa kutafuta, kupata na kutoa habari na mawazo yao kwa misingi iliyo sawa na watu wengine na kwa

kutumia aina zote za mawasiliano wanazozichagua, kama ilivyofafanuliwa katika Ibara ya 2 ya Mkataba huu, ikiwa ni pamoja na:

(a) Habari zinazoulenga umma kuwafikia watu wenye ulemavu kwa njia wanazoweza kupokelea taarifa na teknolojia sadifu kwa aina mbalimbali za ulemavu bila kuchelewa wala kuingia gharama za ziada;

(b) Kurasimisha na kuwezesha matumizi ya lugha ya alama, maandishi ya nukta nundu, nyenzo za kukuza mawimbi ya sauti na mawasiliano mbadala na aina nyinginezo zinazofikika, mifumo na aina za mawasiliano watakayoamua kutumia watu wenye ulemavu katika mawasiliano rasmi;

(c) Kuzihimiza taasisi binafsi zinazohudumia umma, ikijumuisha njia za intaneti, kutoa habari na huduma kwa njia na mifumo itayowawezesha watu wenye ulemavu kuzifikia na kuzitumia huduma hizo;

(d) Kuvihimiza vyombo vya habari, ikijumuisha na wanaosambaza habari kupitia intaneti, kuzifanya huduma zao kuweza kufikiwa na watu wenye ulemavu;

(e) Kutambua na kuendeleza matumizi ya lugha za alama.

## Ibara ya 22
## Kuheshimu faragha

1. Hapana mtu mwenye ulemavu, bila kujali sehemu anayoishi au mpangilio wa makazi, ambaye faragha, familia, nyumba, maandishi yake ama aina nyingine za mawasiliano, vitaingiliwa kiholela au kinyume cha sheria ambapo hadhi na sifa zake vitajeruhiwa. Watu wenye ulemavu wana haki ya kulindwa kisheria dhidi ya kuingiliwa kwa aina ile au kushambuliwa kinyume cha sheria.

2. Waliouridhia Mkataba huu watalinda faragha ya taarifa binafsi, afya na marekebisho ya watu wenye ulemavu kwa misingi ya usawa na watu wengine.

## Ibara ya 23
## Kuheshimu maisha ya kifamilia na familia

1. Nchi zilizoridhia Mkataba huu, zitachukua hatua madhubuti ili kukomesha ubaguzi dhidi ya watu wenye ulemavu katika masuala yote ya ndoa, familia, uzazi na mahusiano ya kimapenzi kwa misingi ya usawa na wengine na kuhakikisha kwamba:

(a) Haki ya watu wote wenye ulemavu waliofikia umri wa kufunga ndoa, na kuanzisha familia kwa misingi huru na ridhaa ya wahusika inatambuliwa;

(b) Haki za watu wenye ulemavu kuamua kwa uhuru na kiuwajibikaji, idadi na mpangilio wa uzazi na kupata taarifa zinazowafaa wanarika, elimu ya uzazi na mpango wa uzazi inatambuliwa, na njia muhimu za kuwawezesha kuzitumia haki hizi zinatolewa;

(c) Watu wenye ulemavu, ikiwa ni pamoja na watoto, wanabaki na kizazi kwa misingi iliyo sawa na watu wengine.

2. Waliouridhia Mkataba huu watahakikisha kuwa, haki na dhamana za watu wenye ulemavu kuhusiana na masuala ya ulezi, ulinzi, udhamini, kuasili watoto na hali kama hizo, au taasisi kama hizo, ambapo maudhui kama haya yamo kwenye sheria za nchi, kwa vyovyote vile maslahi ya mtoto ndiyo yatakayopewa umuhimu. Waliouridhia Mkataba watatoa msaada unaofaa kwa watu wenye ulemavu katika kutekeleza jukumu lao la kulea watoto wao.

3. Waliouridhia Mkataba huu watahakikisha kwamba watoto wenye ulemavu wanakuwa na haki sawa kuhusu maisha ya kifamilia. Ili kuzipata haki hizi, na kuzuia ufichaji, utupaji utelekezaji na ubaguzi wa watoto wenye ulemavu, Waliouridhia Mkataba huu watatoa taarifa mapema na kwa ukamilifu, kuhusu huduma na msaada kwa watoto wenye ulemavu na familia zao.

4. Waliouridhia Mkataba huu watahakikisha kwamba mtoto hataondoshwa kwa wazazi wake bila ya ridhaa yake, isipokuwa pale ambapo mamlaka yenye dhamana ya kufanya hivyo kwa kupitia chombo cha mahakama, itakapoamua kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa, kwamba kuondoshwa huko ni kwa lazima na ni kwa maslahi ya mtoto. Kwa vyovyote vile, mtoto hataondoshwa kwa wazazi wake kwa misingi ya ulemavu, uwe wa mtoto mwenyewe, mmoja kati ya wazazi wake au wazazi wote wawili.

5. Waliouridhia Mkataba huu watafanya kila jitihada, endapo famlia haiwezi kumlea mtoto mwenye ulemavu, kumpatia malezi mbadala ndani ya familia pana, na hilo likishindikana, basi ndani ya jamii katika mazingira ya kifamilia.

## Ibara ya 24
## Elimu

1. Waliouridhia Mkataba huu, wanatambua haki za watu wenye ulemavu kupata elimu. Ili haki hii ipatikane bila ya ubaguzi na kwa misingi ya usawa wa fursa, Waliouridhia Mkataba, watahakikisha kuwepo kwa mfumo wa elimu jumuishi katika ngazi zote na mfumo wa ujifunzaji kwa maisha yote ukijielekeza kwenye:

(a) Uendelezaji kamili wa uwezo wa binadamu na uzingatiaji wa hadhi na kujithamini, kuimarisha hali ya kuheshimu haki za binadamu, uhuru wa kujiamulia na uanuwai miongoni mwa binadamu.

(b) Watu wenye ulemavu kujiendeleza kadri wawezavyo kihaiba, kivipawa na kiubunifu, kadhalika na uwezo wao kiakili na kimwili;

(c) Kuwawezesha watu wenye ulemavu kushiriki ipasavyo katika jamii iliyo huru.

2. Ili haki hii ipatikane, Waliouridhia Mkataba huu watahakisha kwamba:

(a) Mfumo wa elimu hauwatengi watu wenye ulemavu na

kwamba watoto wenye ulemavu hawabaguliwi kwenye elimu ya msingi ambayo ni ya lazima au ile ya sekondari kwa misingi ya ulemavu;

(b) Watu wenye ulemavu wanaweza kuipata elimu ya msingi na ya sekondari katika mfumo jumuishi, bora na bila ya malipo kwa misingi ya usawa na wengine katika jamii waishimo.

(c) Marekebisho stahili yanafanyika kulingana na mahitaji binafsi;

(d) Watu wenye ulemavu wanapata usaidizi unaohitajika ndani ya mfumo wa elimu, ili kuwawezesha kuelimika vilivyo;

(e) Hatua za makusudi za kumuwezesha mtu binafsi mwenye ulemavu zinachukuliwa katika mazingira yanayomuwezesha kufikia upeo wa maendeleo ya kitaaluma na kijamii kama lilivyo lengo la ujumuishaji kamilifu;

3. Nchi zilzoridhia Mkataba huu, zitawawezesha watu wenye ulemavu kujifunza maishani na stadi za kimaendeleo katika jamii ili kurahisisha ushiriki wao ulio kamilifu katika nyanja ya elimu na kama wanajamii wengine. Ili kufikia lengo hili, Waliouridhia Mkataba huu watachukua hatua zinazofaa, zikijumuisha:

a) Kuwezesha mafunzo ya maandishi ya nukta nundu, maandishi mbadala na njia za kukuza mawimbi ya sauti na nyinginezo za kuboresha mawasiliano, mbinu kabilifu za ujongeaji, na kuwezesha huduma za makundi rika na ushauri;

b) Kuwezesha mafunzo ya lugha ya alama na kukuza utambulisho wa kiisimu wa jamii ya viziwi;

c) Kuhakikisha kwamba elimu kwa watu wenye ulemavu, hususan watoto wasioona, viziwi au viziwi wasioona, inatolewa kwa lugha, mfumo na njia sadifu za kimawasiliano, na katika mazingira yatakayotoa nafasi kubwa ya maendeleo kitaaluma na kijamii.

4. Ili kusaidia katika kuhakikisha upatikanaji wa haki hii, Waliouridhia Mkataba huu watachukua hatua madhubuti katika, kuajiri walimu, wakiwemo walimu wenye ulemavu, walio na utaalamu wa lugha ya alama na/au nukta nundu na pia kuwafundisha wataalamu na watumishi katika ngazi zote za elimu. Mafunzo kama hayo yatajumuisha mwamko kuhusu ulemavu na kutumia njia za kukuzia mawimbi ya sauti na zile mbadala kimawasiliano, mbinu na vifaa vya kimafunzo vitakavyowasaidia watu wenye ulemavu.

5 Waliouridhia Mkataba huu, watahakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanapata elimu ya juu, mafunzo ya ufundi, elimu ya watu wazima na mafunzo wakati wote wa maisha yao bila ya ubaguzi wa aina yoyote na kuipata kwa misingi sawa na watu wengine. Ili kufikia hatua hii, Waliouridhia Mkataba huu watahakikisha kwamba marekebisho stahiki yanafanyika kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

## Ibara ya 25
## Afya

Waliouridhia Mkataba huu wanatambua kwamba watu wenye ulemavu wanayo haki ya kunufaika kwa kiwango cha juu cha huduma za afya kinachoweza kupatikana bila ya ubaguzi wowote kwa misingi ya ulemavu. Nchi Wanachama zitachukua hatua zote zinazostahiki katika kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanapata huduma za afya zenye kuzingatia jinsia, ikiwa ni pamoja na zinazohusiana na utengamanisho. Kwa makusudi kabisa Nchi Wanachama:

(a) Zitawapatia watu wenye ulemavu matibabu ya aina, ubora na viwango vile vile vya huduma na mipango ya afya isiyo na/au yenye gharama nafuu kama zinavyotolewa kwa watu wengine, zikijumuisha maeneo ya afya ya uzazi na ile iliyojikita kwenye idadi ya watu na mipango ya elimu ya afya kwa umma.

(b) Zitatoa huduma za afya zinazohitajika kwa watu wenye ulemavu hasa kutokana na ulemavu wao, ikijumuisha utambuzi wa

mapema na kuanzisha afua stahiki na huduma zenye lengo la kupunguza na kuzuia ulemavu zaidi miongoni mwa watoto na watu wazima.

(c) Zitatoa huduma hizo katika maeneo ya karibu na jamii za watu kadri inavyowezekana, yakiwemo maeneo ya vijijini;

(d) Zitawataka wataalamu wa afya kutoa huduma za kiwango sawa kwa watu wenye ulemavu kama zinavyotolewa kwa watu wengine, ikiwa ni pamoja na misingi ya kutoa ridhaa kwa uhuru na ufahamu wa kutosha kadhalika na kuongeza ufahamu wa masuala ya haki za binadamu, hadhi, uhuru na mahitaji ya watu wenye ulemavu kwa njia ya mafunzo na kutangaza viwango vya maadili ya kitabibu kwa taasisi za umma na za binafsi.

(e) Zitakataza ubaguzi dhidi ya watu wenye ulemavu katika utoaji wa bima za afya, na bima za maisha pale ambapo bima kama hizo zinaruhusiwa kisheria katika nchi husika; ambapo zitatolewa kwa misingi ya haki na namna inayofaa.

(f) Zitazuia kumkatalia mtu matibabu na huduma za kiafya kibaguzi au kumnyima chakula na vinywaji kwa misingi ya ulemavu.

**Ibara ya 26**
**Marekebisho na utengamao**

1. Waliouridhia Mkataba huu watachukua hatua madhubuti na sadifu ikiwa ni pamoja na kwa njia ya wanarika kusaidiana, kumuwezesha mtu mwenye ulemavu kufikia na kuendeleza hali ya kujitegemea, kupata uwezo wa kimwili, kiakili, kijamii na kiufundi, pia na kujumuika katika masuala yote ya maisha. Ili kufikia lengo hili, Waliouridhia Mkataba huu wataandaa, kuimarisha na kupanua huduma za marekebesho na utengamao hususani katika nyanja za afya, ajira, elimu na huduma za kijamii kiasi kwamba huduma na programu:

a) Zianze katika hatua za awali kadri itavyowezekana, na zipanue wigo wa upimaji ili kugusa mahitaji na uwezo wa mhusika binafsi;

b) Zinasaidia ushiriki na ujumuishwaji wa wahusika katika jamii na kwenye masuala yote ya jamii, ni za hiari na kwa`kadri inavyowezekana, zinawafikia watu wenye ulemavu katika maeneo yaliyo karibu na jamii zao, ikiwa ni pamoja na maeneo ya vijijini;

2. Nchi Wanachama zitakuza maendeleo ya awali na kuendelea kutoa mafunzo kwa ajili ya wataalamu na watumishi wanaofanyakazi katika fani za marekebisho na utengamao;

3. Nchi Wanachama zitakuza upatikanaji maarifa na matumizi ya vifaa saidizi na teknolojia vilivyosanifiwa kwa ajili ya watu wenye ulemavu kwa kadri vinavyohusiana na marekebisho na utengamanisho.

## Ibara ya 27
## Kazi na Ajira

Waliouridhia Mkataba huu, wanatambua haki ya watu wenye ulemavu kuajiriwa na kufanya kazi kwa misingi sawa na wengine. Hii inajumuisha haki ya fursa ya kujipatia riziki kwa kufanya kazi walizozichagua au kuzikubali wao wenyewe katika soko la ajira, na mazingira yaliyo wazi, jumuishi na yanayofikika kwa watu wenye ulemavu. Waliouridhia Mkataba huu watalinda na kukuza ufanikishaji wa haki ya kufanya kazi, ikijumuisha wale wanaopata ulemavu wakiwa kazini, kwa kuchukua hatua zinazofaa, ikiwa ni pamoja na sheria ili kuweza:

(a) Kukataza ubaguzi kwa msingi wa ulemavu katika mambo yote yanayohusu aina zote za kazi, ikijumuisha masharti ya kuajiri, uajiri na ajira, kudumu kazini, kupandishwa daraja na mazingira ya kazi yaliyo salama kiafya.

(b) Kulinda haki za watu wenye ulemavu, kwa misingi ya usawa na wengine, masharti ya kazi yaliyo adilifu na ya kufaa, ikijumuisha fursa sawa na malipo sawa kwa kazi iliyo na uzito ule ule, mazingira ya kufanyia kazi yaliyo salama kiafya ikiwa ni pamoja na kulindwa dhidi ya manyanyaso, na kusuluhisha migogoro;

(c) Kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanaweza kutumia haki zao mahali pa kazi na vyama huru vya wafanyakazi kwa misingi sawa na wengine.

(d) Kwa namna inayofaa, watu wenye ulemavu kunufaishwa na programu zinazohusiana na teknolojia ya jumla na ushauri wa kiufundi, huduma za mafunzo kazini, na ya kiufundi na mengineyo endelevu.

(e) Kuongeza fursa za ajira na kupandishwa madaraja kwa watu wenye ulemavu katika soko la ajira, pamoja na kusaidiwa, kupata, kudumishwa na kurejeshwa kazini.

(f) Kuimarisha na kukuza fursa za watu wenye ulemavu kujiajiri wenyewe, kuanzisha na kuendesha shughuli za ujasiriamali, kuanzisha vyama vya ushirika na mtu binafsi kujianzishia biashara zake;

(g) Kuajiri watu wenye ulemavu katika sekta ya umma;

(h) Kukuza hali ya watu wenye ulemavu kuajiriwa katika sekta binafsi kwa kuwa na sera na mipango mingine inayofaa ikiwa ni pamoja na ile sera ikibali, utoaji motisha na afua nyinginezo;

(i) Kuhakikisha kwamba marekebisho stahiki yanafanyika mahali pa kazi kwa ajili ya watu wenye ulemavu;

(j) Kukuza upatikanaji wa uzoefu wa watu wenye ulemavu katika soko wazi la ajira;

(k) Kukuza mafunzo ya kitaaluma na stadi za kiufundi, kudumu kazini na mipango maalum ya watu wenye ulemavu kurudishwa kazini.

2. Waliouridhia Mkataba huu, watahakikisha kwamba watu wenye ulemavu hawafanywi watumwa au watwana na wanalindwa kwa misingi ya usawa na watu wengine dhidi ya ajira za kushurutishwa au za lazima.

**Ibara ya 28**
**Ubora wa maisha na hifadhi ya kijamii**

1. Waliouridhia Mkataba huu wanatambua haki ya watu wenye ulemavu ya kupata maisha bora wao wenyewe na familia zao, ikiwa ni pamoja na chakula , mavazi na makazi, na muendelezo wa hali bora ya maisha, na zitachukua hatua mathubuti kulinda na kuendeleza upatikanaji wa haki hii bila ya ubaguzi kwa misingi ya ulemavu.

2. Waliouridhia Mkataba huu wanatambua haki ya watu wenye ulemavu kupata hifadhi ya kijamii na kufaidika na haki hiyo bila ya ubaguzi kwa msingi wa ulemavu, na zitachukua hatua stahiki katika kulinda na kukuza haki hiyo ikijumuisha hatua kama vile:

(a) Kuhakikisha kwamba huduma za maji safi, na kuhakikisha kwamba huduma zinazofaa na zenye gharama nafuu, visaidizi na usaidizi mwingine unaohusiana na mahitaji ya ulemavu zinawafikia watu wenye ulemavu kwa misingi ya usawa;

(b) Kuhakikisha kwamba mipango ya hifadhi ya jamii na ile ya kupunguza umasikini inawafikia watu wenye ulemavu, hususan, wanawake, wasichana na wazee wenye ulemavu;

(c) Kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu na familia zao wanaoishi katika hali ya umasikini wanapata huduma moja kwa moja kutoka serikalini, ikiwa ni pamoja na gharama zinazohusiana na ulemavu kama vile mafunzo ya kutosha, ushauri nasaha, ruzuku na matunzo wakati wa fadhaa zinazotokana na ulemavu, maumivu na msendeko.

(d) Kuhakikisha kwamba programu za umma za makazi zinawafikia watu wenye ulemavu;

(e) Kuhakikisha kwamba programu za mafao ya uzeeni zinawafikia watu wenye ulemavu katika misingi ya usawa.

**Ibara ya 29**

## Kushiriki katika Siasa na Kuhudumia Umma

Waliouridhia Mkataba huu wanawahakikishia watu wenye ulemavu haki za kisiasa na fursa ya kunufaika na haki hizo kwa misingi ya usawa na watu wengine, na zitachukua hatua za:

(a) Kutoa hakikisho kuwa watu wenye ulemavu wanaweza kushiriki kwa ukamilifu katika medani ya siasa na huduma kwa umma kwa misingi iliyo sawa na wengine moja kwa moja au kwa kupitia wawakilishi waliochaguliwa kwa misingi huru, ikiwa ni pamoja na fursa ya watu wenye ulemavu kupiga kura na kuchaguliwa, pamoja na mengine kwa:

(i) Kuhakikisha kwmba utaratibu wa kupiga kura, vifaa na nyenzo ni sadifu, vinafikika, na vinaeleweka na kutumika kwa urahisi;.

(ii) Kulinda haki ya watu wenye ulemavu kupiga kura kwa siri wakati wa uchaguzi na bila kudhalilishwa, na kugombea, kuchukua dhamana za uongozi na kutekeleza masuala yote ya umma katika ngazi zote za serikali, kuwezesha matumizi ya visaidizi na teknolojia mpya kama itavyoonekana inafaa;

(iii) Kutoa hakikisho la uhuru wa maoni kwa watu wenye ulemavu kama wapiga kura, na katika kulifanya hili liwezekane pale inapobidi, mhusika ataomba, na kuruhusiwa kusaidiwa kupiga kura yake na mtu aliyemteua mwenyewe;

(b) Kukuza mazingira ambamo watu wenye ulemavu wanaweza kushiriki kikamilifu katika masuala ya umma bila ya ubaguzi, na kwa misingi ya usawa na wengine, na kuhimiza ushiriki wao katika mambo ya umma, ikijumuisha:

(i) Kushiriki katika asasi za kiraia na zile zinazojihusisha na masuala ya umma na siasa za nchi, na katika shughuli na uongozi wa vyama vya siasa;

(ii) Kuunda na kujiunga na vyama vya watu wenye ulemavu ili kuwawakilisha katika ngazi za kimataifa, kitaifa, kikanda na kimitaa.

## Ibara ya 30
## Kushiriki katika masuala ya kitamaduni, mapumziko, burdani na michezo

1. Waliouridhia Mkataba huu wanatambua haki ya watu wenye ulemavu kushiriki kwa msingi wa usawa na watu wengine katika mambo ya kitamaduni, na zitachukua hatua zinazofaa ili kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu:

(a) Wanafaidika na fursa za kupata vifaa vya kitamaduni kwa njia zinazofikika;

(b) Wanafaidika na vipindi vya televisheni, filamu, michezo ya kuigiza na shughuli nyingine za kitamaduni kwa njia anuwai zinazowafaa.

(c) Wanafaidika bila vikwazo, sehemu zinapofanyikia shughuli au huduma za kitamaduni kama vile kumbi za maonyesho, makumbusho, sinema, maktaba na huduma za kitalii, na kadri inavyowezekana, kuyafikia majengo ya kihistoria, na sehemu nyingine umuhimu kwa utamaduni wa jamii.

2. Waliouridhia Mkataba huu watachukua hatua zinazofaa kuwawezesha watu wenye ulemavu kuwa na fursa ya kujiendeleza na kutumia ubunifu, usanii na uwezo wao kiakili, siyo tu kwa manufaa yao, bali pia kwa ustawishaji wa jamii .

3. Waliouridhia Mkataba huu watachukua hatua madhubuti, kwa mujibu wa sheria za kimataifa, katika kuhakikisha kuwa sheria zinazolinda haki za ubunifu, haziweki vikwazo au kuwabagua watu wenye ulemavu katika kupata vifaa vya kitamaduni.

4. Watu wenye ulemavu wanakuwa na haki, kwa msingi wa usawa na watu wengine, kutambuliwa na kuunga mkono masuala yao mahususi ya kitamaduni na utambulisho kiisimu; ikijumuisha lugha ya alama na utamaduni wa viziwi.

5. Ili kuwawezesha watu wenye ulemavu kushiriki kwa msingi wa usawa na watu wengine katika mapumziko, shughuli za burudani na michezo, Waliouridhia Mkataba huu watachukua hatua zifaazo:

(a) Kuhimiza na kuendeleza watu wenye ulemavu katika kushiriki, kwa kadri iwezekanavyo, kwenye michezo ngazi zote;

(b) Kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanakuwa na fursa ya kuandaa, kuendeleza na kushiriki kwenye riadha na burudani ambavyo ni mahsusi kwa watu wenye ulemavu. Hali hii itafikiwa kwa kushajiisha uwekaji masharti ya mafunzo, ufundishaji na rasilimali zinazofaa kwa msingi wa usawa na watu wengine;

(c) Kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanaweza kufika maeneo ambapo michezo, burudani na shughuli za kitalii vinakofanyikia,

(d) Kuhakikisha kuwa watoto wenye ulemavu wanapata nafasi sawa na wenzao ya kushiriki katika michezo, mapumziko na burdani, na shughuli zote za michezo ikijumuisha ile iliyo kwenye mfumo wa kishule;

(e) Kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanapata huduma kutoka kwa wale wanaoandaa shughuli za mapumziko, utalii, burudani na michezo.

## Ibara ya 31
## Takwimu na Ukusanyaji wa taarifa

1. Nchi Wanachama zinaahidi kukusanya taarifa muhimu, ikiwa ni pamoja na takwimu na taarifa zilizofanyiwa utafiti ili kuziwezesha kuandaa na kutekeleza sera, kwa nia ya kukidhi matakwa ya Mkataba huu. Mchakato wa kukusanya na kuzihifadhi taarifa utahusisha:

a) Kuzingatia kinga zilizowekwa kisheria ikijumuisha sheria ya kuhifadhi taarifa, katika kuhakikisha usiri na kuheshimu faragha ya watu wenye ulemavu;

b) Kuzingatia kanuni zinazokubalika kimataifa za kulinda haki za binadamu na uhuru wa msingi na maadili yanayotumika katika ukusanyaji na utumiaji takwimu.

2. Taarifa zilizokusanywa kwa mujibu wa ibara hii, zitachambuliwa kwa kadri inavyofaa na zitatumiwa kufanyia tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya nchi zilizouridhia Mkataba huu na kutambua na kushughulikia vikwazo vinavyowakabili watu wenye ulemavu katika kutumia haki zao.

3. Waliouridhia Mkataba huu watabeba dhamana ya kusambaza takwimu hizi na kuhakikisha kuwa zinapatikana bila vikwazo kwa watu wenye ulemavu na wengineo.

## Ibara ya 32
## Ushirikiano wa kimataifa

1. Waliouridhia Mkataba huu wanatambua umuhimu wa ushirikiano wa kimataifa na uendelezaji wake katika kuunga mkono juhudi za kitaifa za kuyafikia makusudio na malengo ya Mkataba huu, na zitachukua hatua madhubuti kwa minajili hii, baina na miongoni mwa mataifa na kwa kadri inavyofaa kwa ubia na jumuiya za kimataifa na za kikanda na zile za kiraia, hususan, vyama/asasi za watu wenye ulemavu. Hatua za aina hiyo zinaweza kujumuisha:

(a) Kuhakikisha kwamba ushirikiano wa kimataifa, ikiwemo mipango ya maendeleo ya kimataifa inawajumuisha na kuwafikia watu wenye ulemavu;

(b) Kuwezesha na kuunga mkono mipango ya kujenga uwezo, ikiwa ni pamoja na kubadilishana taarifa, uzoefu, mipango ya mafunzo na mazoea mema yanayofaa kuigwa;

(c) Kuwezesha ushirikiano wa kitafiti na ufikiwaji wa taarifa za kisayansi na kiteknolojia;

(d) Kutoa, kwa kadri inavyofaa, msaada wa kiufundi na kiuchumi, ikijumuisha kuwezesha ufikiaji na ushirikishanaji wa teknolojia saidizi iliyopo kwa njia ya na uhawilishaji wa teknolojia.

2. Vipengele vya ibara hii haviathiri utekelezaji wa majukumu ya Mkataba huu kwa kila nchi iliyouridhia.

## Ibara ya 33
## Utekelezaji na ufuatiliaji ngazi ya Kitaifa

1. Kwa mujibu wa muundo wa kila nchi iliyoridhia Mkataba huu zitajipangia eneo moja au zaidi ambayo ni mahususi kwa ajili ya masuala yanayohusiana na utekelezaji wa Mkataba huu ndani ya serikali na itazingatia uanzishaji wa mfumo wa kuratibu hatua zinazohusu utekelezaji wa kisekta katika ngazi mbalimbali serikalini .

2. Kwa mujibu wa miundo ya kisheria na kiutawala, Waliouridhia Mkataba huu, watadumisha, wataimarisha, watadhihirisha, au kuanzisha nchini, muundo mmoja au zaidi, ulio huru kwa kadri inavyofaa ili kuendeleza, kulinda na kufuatilia utekelezaji wa Mkataba huu. Wakati wa kuanzisha muundo huo, waliouridhia Mkataba huu, watazingatia kanuni zinazohusiana na hali ya utendaji kazi wa taasisi za kitaifa katika kulinda na kukuza haki za binadamu.

3. Asasi za kiraia, hususan zile za watu wenye ulemavu na vyama vinavyowawakilisha vitashirikishwa na kushiriki kwa ukamilifu kwenye mchakato wa ufuatiliaji.

## Ibara ya 34
## Kamati kwa ajili ya Haki za Watu wenye Ulemavu

1. Itaanzishwa Kamati ya Kimataifa kuhusu Haki za Watu Wenye Ulemavu (halafu itajulikana kama “Kamati”) itakayofanya kazi zitakazofafanuliwa.

2. Wakati wa kurasmisha Mkataba huu, itakuwepo Kamati yenye wataalamu kumi na wawili. Pale nchi sitini au zaidi zitakapouridhia au kuukubali Mkataba huu, Kamati hii itapanuliwa kwa kuongezewa wajumbe wengine sita na hivyo, kufikia ukomo wa wajumbe kumi na wanane.

3. Wajumbe wa Kamati wataitumikia wakiwa na dhamana binafsi na ni wale ambao wametukuka kiuadilifu, kiubingwa na kiuzoefu katika masuala yaliyomo kwenye Mkataba huu. Nchi Wanachama zitateua wagombea wao kwenye kamati hii kwa kuzingatia matakwa yaliyomo katika Ibara ya 4, aya ya 3 ya Mkatabu huu.

4. Wajumbe wa Kamati watachaguliwa na Nchi zilizoridhia Mkataba huu kwa kutilia maanani uwiano wa mgawanyo kijiografia, uwakilishi wa aina tofauti za ustaarabu na mifumo mikuu ya kisheria, mizania ya kijinsia na ushiriki wa mabingwa wenye ulemavu.

5. Wajumbe wa Kamati hii watachaguliwa kwa kura ya siri kutokana na orodha ya wajumbe waliopendekezwa na mikutanao ya jumuiko la Waliouridhia Mkataba huu Katika majumuiko hayo ambayo akidi yake ni theluthi mbili ya Waliouridhia Mkataba huu, watu watakaochaguliwa kuwa wanakamati watakuwa ni wale waliopata idadi kubwa zaidi ya kura zilizopigwa kwa uhuru kabisa na wengi wa wawakilishi wa Waliouridhia Mkataba huu waliohudhuria na kushiriki uchaguzi.

6. Uchaguzi wa awali utafanyika si zaidi ya miezi sita baada ya Mkataba huu kuanza kufanya kazi rasmi. Angalau miezi minne kabla ya tarehe ya kufanyika kwa uchaguzi wowote ule, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, ataziandikia barua Waliouridhia Mkataba huu akikaribisha mapendekezo ya majina ambayo yatawasilishwa kwake katika kipindi cha miezi miwili baada ya taarifa. Kisha, Katibu Mkuu ataandaa orodha ya watu wote walioteuliwa katika mfumo wa kialfabeti, na akiainisha nchi zilizowapendekeza na kuiwasilisha mbele ya Waliouridhia Mkataba huu.

7. Wanakamati watachaguliwa kwa vipindi vya miaka minne minne. Wanaweza kuchaguliwa tena kwa muhula mwingine mmoja tu. Hata hivyo, dhamana ya wanakamati sita waliochaguliwa katika uchaguzi wa mwanzo, utakoma kufuatia uchaguzi utakaofanyika baada ya kipindi cha miaka miwili tangu ule wa mwanzo. Mara baada ya uchaguzi wa kwanza, majina ya wanakamati hao sita yatachaguliwa kwa njia ya kubahatisha na Mwenyekiti wa jumuiko lililozungumziwa katika aya ya tano ya ibara hii.

8. Uchaguzi wa wanakamati sita wa ziada utafanyika wakati wa uchaguzi wa kawaida, kwa mujibu wa vifungu husika kwenye Ibara hii.

9. Endapo mwanakamati atafariki dunia au kujiuzulu au atatamka mwenyewe kwamba kwa sababu fulani fulani hawezi tena kuendelea kutekeleza majukumu yake, Nchi iliyoridhia Mkataba huu ambayo ilimpendekeza kwa mara ya kwanza, itamteua bingwa mwingine mwenye sifa na kutosheleza vigezo vilivyobainishwa na vifungu husika vya ibara hii, ili atumikie muda uliobakia.

10. Kamati itatayarisha utaratibu wake wa kazi.

11. Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa atatoa wafanyakazi na vifaa vinavyotakiwa katika kutekeleza kiufanisi kazi za kamati chini ya Mkataba huu, na mkutano wa kuizindua Kamati atauitisha yeye.

12. Kwa idhini ya Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, wajumbe wa Kamati iliyoundwa chini ya Mkataba huu, watapata ujira kutokana na rasilimali za Umoja wa Mataifa kwa mujibu wa matakwa na masharti yanayoweza kuamuliwa na Baraza Kuu likitilia maanani umuhimu wa majukumu ya Kamati;

13. Wajumbe wa Kamati watakuwa na haki ya kupata vitendea kazi, marupurupu na kinga kama ilivyo kwa mabingwa wengine kwenye ujumbe wa Umoja wa Mataifa kama inavyofafanuliwa kwenye vifungu husika vya Mkataba wa marupurupu na kinga za Umoja wa Mataifa.

## Ibara ya 35
## Taarifa za Waliouridhia Mkataba huu

1. Kupitia kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kila aliyeuridhia Mkataba huu atawasilisha mbele ya Kamati, taarifa ya kina ya hatua zilizochukuliwa katika kutimiza wajibu wake chini ya Mkataba huu na maendeleo yaliyopatikana kutokana na utekelezaji huo ndani ya muda wa miaka miwili baada ya kuanza kutumika rasmi katika kila aliyeuridhia.

2. Kuanzia hapo, kila aliyeuridhia Mkataba huu, atawasilisha taarifa zake walau kila baada ya miaka minne au zaidi kwa kadri Kamati itavyoitaka.

3. Kamati itaamua, aina ya miongozo itakayotumika kwenye maudhui ya taarifa.

4. Kila aliyeuridhia Mkataba huu aliyewasilisha taarifa yake ya kina mbele ya Kamati, hatakuwa na haja ya kurudia mambo yale yaliyokwisha taarifiwa awali. Katika kutayarisha taarifa kwa ajili ya Kamati Waliouridhia Mkataba huu wanatakiwa kuzingatia kufanya hivyo kwa kutumia mchakato wenye uwazi na kutilia maanani matakwa yaliyomo katika Ibara ya 4, aya ya 3 ya Mkataba huu.

5. Ripoti zinaweza kubainisha sababu na changamoto zinazoathiri kiwango cha utekelezaji wa majukumu chini ya Mkataba huu.

## Ibara ya 36
## Kujadili taarifa

1. Kamati, itazingatia kila taarifa na itatoa ushauri na mapendekezo ya jumla kuhusu taarifa yenyewe kama itakavyoona inafaa na kuiwasilisha kwa mhusika. Mhusika anaweza kujibu kwa kutoa maelezo yoyote kwa

Kamati. Pia Kamati inaweza kutaka maelezo ya ziada yanayohusiana na utekelezaji wa Mkataba huu kutoka kwa mhusika.

2. Ikiwa aliyeridhia Mkataba huu atakawia sana kuwasilisha taarifa yake, Kamati inaweza kumuarifu juu ya umuhimu wa kukagua hali ya utekelezaji wa Mkataba huu kwa mujibu wa maelezo ya kuaminika yaliyoifikia Kamati. Ikiwa taarifa inayotakiwa, haitawasilishwa ndani ya miezi mitatu baada ya kukumbushiwa, Kamati itamwalika mhusika kushiriki katika uchunguzi huo. Ikiwa mhusika hatajibu kwa kuwasilisha taarifa inayohitajika na matakwa ya aya ya 1 ya ibara hii yatatumika.

3. Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa atasambaza taarifa hizi kwa wote waliouridhia Mkataba huu.

4. Waliouridhia Mkataba huu, watausambazia umma taarifa zake zinazohusu nchi yao kadhalika na ushauri na mapendekezo ya jumla kuhusiana na taarifa yenyewe.

5. Kamati itazituma, fedha na programu za Umoja wa Mataifa kwa wakala maalum na jumuiya nyingine kwa kadri itakavyoona inafaa, ili zikashughulikie ombi au dalili za haja ya ushauri wa kiufundi au msaada, pamoja na ushauri wa Kamati na mapendekezo, kama yapo, juu ya maombi hayo au dalili hizo.

## Ibara ya 37
## Ushirikiano baina ya Waliouridhia Mkataba huu na Kamati

1. Kila aliyeuridhia Mkataba huu huu itashirikiana na Kamati na kuwasaidia wajumbe wake kutekeleza wajibu wao.

2. Katika uhusiano wake na Waliouridhia Mkataba huu, Kamati itazingatia njia na mbinu za kuendeleza uwezo wa kila aliyeuridhia katika kutekeleza Mkataba huu, ikiwa ni pamoja na kwa njia za ushirikiano wa kimataifa.

## Ibara ya 38

## Uhusiano wa Kamati na vyombo vingine

Katika kuendeleza utekelezaji mzuri wa Mkataba huu na kushajiisha ushirikiano wa kimataifa katika maeneo yaliyoainishwa ndani ya Mkataba huu:

a) Wakala za Umoja wa Mataifa zitakuwa na haki ya kuwakilishwa wakati wa kupangilia utekelezaji wa matakwa ya Mkataba yanayoangukia kwenye mamlaka zao. Kamati inaweza kuzialika wakala maalum na vyombo vingine vya kitaalamu kadri itakavyoona inafaa ili vitoe ushauri wa kitaalamu juu ya utekelezaji wa Mkataba huu katika maeneo yanayoangukia kwenye mamlaka zao. Kamati inaweza kuzikaribisha wakala maalum na vyombo vingine vya Umoja wa Mataifa kuwasilisha taarifa zao juu ya utekelezaji wa Mkataba huu katika maeneo yanayoangukia kwenye mamlaka zao;

b) Katika kutekeleza mamlaka iliyonayo, Kamati, kwa kadri itakavyoona inafaa, itashauriana na vyombo vingine vinavyoanzishwa kwa mikataba ya haki za binadamu kwa lengo la kuhakikisha uthabiti wa mfumo wa miongozo ya kutayarisha taarifa husika, maoni na mapendekezo ya jumla na hivyo kujiepusha na marudio na kuingiliana katika utekelezaji wa majukumu yao.

## Ibara ya 39
## Taarifa ya Kamati

Kamati itatoa taarifa ya shughuli zake kila baada ya miaka miwili mbele ya Baraza Kuu na kwa Halmashauri ya masuala ya kiuchumi na kijamii na inaweza kushauri na kutoa mapendekezo ya jumla kutokana na uchunguzi na taarifa ilizozipokea kutoka kwa waliouridhia Mkataba huu. Ushauri huo na mapendekezo ya jumla yataingizwa katika taarifa ya Kamati pamoja na maoni, kama yapo, kutoka kwa waliouridhia.

## Ibara ya 40
## Kikao cha Waliouridhia Mkataba huu

1. Waliouridhia Mkataba huu, watakutana mara kwa mara katika vikao rasmi, ili kushughulikia jambo lolote kuhusu utekelezaji wake.

2. Kabla ya miezi sita kupita tokea Mkataba huu kuanza kutumika rasmi, kikao cha Waliouridhia Mkataba huu kitaitishwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Mikutano itayofuata itaitishwa na Katibu Mkuu kila baada ya miaka miwilimiwili au kwa kutakiwa kufanya hivyo kutokana na maamuzi ya kikao cha Waliouridhia Mkataba huu.

**Ibara ya 41**
**Utunzaji**

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa atakuwa ndiye mtunzaji mkuu wa Mkataba huu.

**Ibara ya 42**
**Saini**

Mkataba huu utawekwa wazi Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa New York, kuanzia Machi 30, 2007 kwa ajili ya kusainiwa na Nchi zote na Jumuiya za Kikanda.

**Ibara ya 43**
**Hiari ya kuwajibika**

Mkataba huu utatakiwa kuridhiwa na Nchi zilizotia saini na kuthibitishwa rasmi kwa saini. Jumuiya za kikanda pia zinaweza kuuridhia Mkataba huu. Mkataba huu utakuwa wazi kupata ridhaa ya nchi yoyote au Jumuiya ya Kikanda ambayo haijasaini Mkataba huu.

**Ibara ya 44**
**Jumuiya za kikanda**

1. "Jumuiya ya Kikanda" itamaanisha taasisi iliyoundwa na Nchi huru katika eneo fulani ambapo Nchi wanachama wamekabidhi uwezo wa kisheria wa masuala yanayolindwa na Mkataba huu. Taasisi za aina hii zitatangaza kwenye vyombo vyake kuthibitisha au kukubali na kufafanua

ukomo wake kisheria kuhusiana na mambo yanayolindwa na Mkataba huu. Halafu zitamuarifu Mtunzaji juu ya mabadiliko yoyote ya msingi yanayohusu uwezo wa kisheria.

2. Pale panapotamkwa "Waliouridhia Mkataba huu" patahusisha pia Jumuiya za aina hii kwa kadri ya ukomo wa uwezo wake kisheria.

3. Kwa madhumuni ya Ibara ya 45, aya ya 1 na ibara ya 47 aya ya 2 na 3 ya Mkataba huu, hati za kuridhia au mapendekezo ya marekebisho toka kwenye Jumuiya za Kikanda hayatazingatiwa.

4. Kulingana na ukomo wa uwezo wa kisheria zilizonao Jumuiya za Kikanda, zinaweza kutumia haki yake ya kupiga kura katika vikao vya Waliouridhia Mkataba huu kwa idadi sawa ya kura na zile Nchi zinazounda Jumuiya husika. Jumuiya hizo hazitatumia haki ya kupiga kura ikiwa mmoja wa Nchi mwanachama wake ametumia haki yake ya kupiga kura, au vinginevyo.

## Ibara ya 45
## Kuanza kutumika rasmi

1. Mkataba huu utaanza kutumika rasmi siku ya thelathini baada ya kupokelewa kwa hati ya ishirini ya kuuridhia au kuukubali.

2. Kwa kila Nchi au Jumuiya ya Kikanda iliyoridhia na kuuthibitisha rasmi au kuukubali Mkataba huu baada ya kuwasilishwa kwa hati ya ishirini, Mkataba huu utaanza kutumika siku ya thelathini baada ya kuwasilishwa kwa hati yake yenyewe.

## Ibara ya 46
## Shaka

1. Shaka lolote lisiloendana na lengo au makusudio ya Mkataba huu halitaruhusiwa.
2. Shaka linaweza kuondolewa wakati wowote.

**Ibara ya 47**
**Marekebisho**

1. Nchi yoyote iliyoridhia Mkataba huu inaweza kupendekeza marekebisho kwenye Mkataba huu na kuyawasilisha kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Katibu Mkuu atawasilisha mapendekezo ya marekebisho yoyote kwa Nchi zilizouridhia Mkataba huu pamoja na ombi la kuzitaka zimjulishe kama zinapendelea kuitishwa kwa jumuiko la Nchi zilizoridhia kwa madhumuni ya kufikiria na kuamua juu ya mapendekezo hayo. Itakapotokea kwamba ndani ya miezi minne tokea tarehe ya mawasiliano hayo angalau theluthi moja ya Nchi zilizoridhia zimependelea kuitishwa kwa kikao, basi Katibu Mkuu atakiitisha chini ya mwavuli wa Umoja wa Mataifa. Marekebisho yoyote yatakayopitishwa kwa wingi wa theluthi mbili ya kura za Nchi zilizohudhuria na kupiga kura, yatawasilishwa na Katibu Mkuu mbele ya Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kwa kuidhinishwa na baadaye kwa Nchi zote zilizoridhia ili ziyakubali.

2. Marekebisho yaliyopitishwa na kuthibitishwa kwa mujibu wa aya ya 1 ya ibara hii, yataanza kutumika siku ya thelathini baada ya hati za kuyakubali zilizowasilishwa kufikia theluthi mbili ya Nchi zilizoridhia siku ya kupitishwa kwa marekebisho. Kisha, marekebisho yataanza kutumika kwa Nchi yoyote siku ya thelathini kufuatia ilipoweka hati yake yenyewe ya kuyakubali. Ni Nchi zile tu zilizoridhia ambazo zimeyakubali marekebisho ndizo zitakazobanwa na marekebisho hayo.

3. Ikiwa itaamuliwa kwa pamoja na kikao cha Nchi zilizoridhia marekebisho yaliyofanywa na kuthibitishwa kwa mujibu wa aya ya 1 ya ibara hii ambayo yanahusiana, hususan, na ibara ya 34, 38, 39 na 40, yataanza kutumika kwa Nchi zote zilizoridhia siku ya thelathini baada ya hati za kuyakubali kufikia theluthi mbili ya idadi ya Nchi zilizoridhia siku ile yalipopitishwa .

**Ibara ya 48**
**Kujitoa**

Nchi iliyoridhia Mkataba huu inaweza kujitoa katika utekelezaji wake kwa kumpelekea Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa taarifa ya maandishi kuhusu kujitoa kwake. Kujitoa huko kutatekelezeka mwaka mmoja baada ya tarehe ambayo Katibu Mkuu alipokea taarifa hiyo.

## Ibara ya 49
## Njia rahisi ya kupatikana

Mkataba huu utaweza kupatikana katika hali zinazofikika.

## Ibara ya 50
## Mkataba Halisi

Nakala za Mkataba huu kwa lugha za Kiarabu, Kichina, Kiingereza, Kifaransa, Kirusi na Kihispania zitakuwa na uhalisia ule ule.

**KWA KUSHUHUDIWA na wajumbe wenye mamlaka kamili** waliosaini hapo chini kwa kuidhinishwa na na Serikali husika wametia saini Mkataba huu.

# Mkataba wa Nyongeza kwa Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu

Walioridhia Mkataba wa Nyongeza wamekubaliana kama ifuatavyo:

## Ibara ya 1

1. Walioridhia Mkataba huu wa Nyongeza wanatambua uwezo wa Kamati ya Haki za Watu wenye Ulemavu (Kamati) wa kupokea na kutafakari taarifa kwa mujibu wa mamlaka yake kutoka kwa au kwa niaba ya watu binafsi au makundi ya watu ambao wanadai kuwa ni waathirika wa

ukiukwaji wa masharti ya Mkataba huu wa Kimataifa ulioridhiwa na mamlaka husika.

2. Hakuna taarifa itakayopokelewa na Kamati ikiwa inaihusu Nchi iliyoridhia Mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu lakini ambayo bado haikuiridhia Mkataba wa Nyongeza.

## Ibara ya 2

Kamati itaichukulia taarifa fulani kwamba haipaswi kushughulikiwa ikiwa:

(a) Taarifa haitambuliki ilikotoka.

(b) Taarifa hiyo itakuwa inakiuka haki ya kuwasilisha taarifa za aina hiyo au haikubaliani na vipengele vya Mkataba;

(c) Suala hilo tayari limeshachunguzwa na Kamati, au linachunguzwa chini ya utaratibu mwingine wa upelelezi au usuluhishi wa kimataifa;

(d) Kabla ya kuzipitia njia zote za kulipatia ufumbuzi tatizo hilo ndani ya Nchi husika. Kipengele hiki hakitokuwa na uzito endapo utatuzi wa tatizo utaonekana kuchukua muda mrefu bila sababu za msingi au kutoelekea kuleta faraja inayofaa;

(e) Taarifa haitakuwa na ithibati au maelezo yenye kujitosheleza, au endapo

(f) Tatizo ambalo ni chanzo cha taarifa litakuwa lilitokea kabla ya Mkataba huu wa Nyongeza kuanza kutumika kwa Nchi iliyoridhia, isipokuwa kama tatizo hilo liliendelea baada ya hapo.

## Ibara ya 3

Kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 2 ya Mkatatba wa Nyongeza, Kamati itawasilisha tuhuma iliyoipokea kwa njia ya siri kwa Nchi iliyoiridhia na inayotuhumiwa. Ndani ya kipindi cha miezi sita, Nchi iliyoridhia itawasilisha mbele ya Kamati maelezo, kwa maandishi au maelezo ya ana kwa ana, ikifafanua jambo linalolalamikiwa na hatua za utatuzi wake, ambazo zimechukuliwa na Nchi husika, kama zipo.

## Ibara ya 4

1. Wakati wowote baada ya kupokea taarifa na kabla ya kufikia uamuzi kwa hoja, Kamati inaweza kuipelekea Nchi iliyoridhia ombi kuchukuliwa kwa hatua za muda mfupi kadri itakavyokuwa ni lazima ili kuepuka athari isiyoweza kurekebishika inayoweza kumpata muathirika au waathirika wa ukiukwaji tuhumiwa.

2. Pale Kamati itakapoamua kutumia mamlaka yake chini ya aya ya kwanza ya ibara hii, haimaanishi kuwa imetoa uamuzi wa kuikubali taarifa au juu ya ustahili wa malalamiko yaliyowasilishwa.

## Ibara ya 5

Katika kujadili malalamiko chini ya Mkataba wa Nyongeza, Kamati itafanya mikutano ya faragha. Baada ya kuchunguza taarifa, Kamati itapeleka ushauri na mapendekezo yake, kama yapo, kwa Nchi husika iliyoridhia na kwa mlalamikaji.

## Ibara ya 6

1. Ikiwa Kamati itapokea taarifa ya kuaminika kwamba Nchi iliyoridhia inafanya ukiukaji mkubwa au ina mfumo unaokiuka haki zilizotamkwa ndani ya Mkataba, Kamati itaitaka Nchi husika kushirikiana nayo katika kuchunguza taarifa, na kwa ajili hiyo, kuwasilisha maoni kuhusu taarifa husika.

2. Kwa kuzingatia maoni yoyote ambayo yamewasilishwa na Nchi husika iliyoridhia pamoja na taarifa nyingine yoyote ya kuaminika iliyopatikana, Kamati inaweza kuteua mjumbe wake mmoja au zaidi kufanya uchunguzi na kutoa taarifa ya haraka kwa Kamati. Endapo itaruhusiwa na kwa ridhaa ya Nchi iliyoridhia, uchunguzi unaweza kujumuisha ziara ndani ya Nchi inayolalamikiwa.

3. Baada ya uchambuzi, Kamati itawasilisha yaliyogunduliwa kwenye uchunguzi huo, mbele ya Nchi husika ikiwa ni pamoja na maoni na mapendekezo yoyote kama yapo.

4. Nchi inayohusika itatakiwa kutoa maoni na mapendekezo kwa Kamati ndani ya kipindi cha miezi sita tokea kupokea taarifa ya uchunguzi;

5. Uchunguzi wa aina hiyo utafanywa kwa siri na kwa kuomba ushirikiano na Nchi husika katika hatua zote za uchunguzi.

## Ibara ya 7

1. Kamati inaweza kuitaka Nchi husika kujumuisha kwenye ripoti yake chini ya Ibara ya 35 ya Mkataba huu, maelezo ya hatua zilizochukuliwa mintarfu uchunguzi uliofanywa chini ya Ibara ya sita ya Mkataba wa Nyongeza.

2. Baada ya kipindi cha miezi sita kilichotajwa katika Ibara ya 6, aya ya 4 kupita ikibidi, Kamati inaweza kuitaka Nchi husika iliyoridhia kuiarifu juu ya hatua ilizochukua kuhusiana na uchunguzi kama huo.

## Ibara ya 8

Kila Nchi iliyoridhia inaweza wakati wa kutia saini au kuridhia, au kuukubali Mkataba wa Nyongeza, kutangaza kuwa haitambui uwezo wa Kamati hii ulioelezwa katika Ibara ya 6 na 7.

## Ibara ya 9

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa atakuwa ndiye Mhifadhi wa Itifaki hii ya Hiari.

**Ibara ya 10**

Mkataba wa Nyongeza utakuwa wazi kwa kutiwa saini na Nchi zilizoridhia na jumuiya za muungano wa kikanda za Mkataba huu wa Kimataifa katika Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa, New York, kuanzia tarehe 30 Machi, 2007.

**Ibara ya 11**

Kuanza kutumika rasmi kwa Mkataba huu wa Nyongeza kutategemeana na kusainiwa na Nchi (zilizotia saini) ambazo zimeridhia au kuukubali Mkataba. Itatakiwa kuthibitishwa rasmi kwa kusaniwa na Jumuiya za Muungano wa Kikanda zilizotia saini mkataba wa Nyongeza ambazo zimethibitisha rasmi au kuukubali Mkataba. Utakuwa wazi kukubaliwa na Nchi au Jumuiya ya Muungano wa Kikanda yoyote ambayo imeridhia, imethibitisha rasmi au kuukubali Mkataba na ambayo haijatia saini mkataba wa Nyongeza.

**Ibara ya 12**

1. "Jumuiya za Muungano wa Kikanda" zitamaanisha jumuiya zilizoundwa na Nchi huru za eneo fulani la kijiografia ambapo wanajumuiya (nchi zinazoiunda) zitakasimu mamlaka yanayotawaliwa na Mkataba huu kadhalika na Mkataba wa Nyongeza. Jumuiya za aina hii zitatamka kupitia hati rasmi za uthibitishaji au ukubalifu kiwango cha mamlaka kuhusiana na mambo yanayoongozwa na Mkataba na Mkataba wa Nyongeza kadhalika. Halafu zitamuarifu Mhifadhi pale yatakapotokea mabadiliko yoyote ya msingi yanayohusu uwezo wake;

2. Kwa mujibu wa Mkataba huu wa Nyongeza Jumuiya kama hizo zitatajwa kama "Nchi zilizoridhia" kulingana na mipaka yake ya kiuwezo;

3. Kwa madhumuni ya ibara ya 13, aya ya 1 na ibara ya 15 aya ya 2 ya Mkataba huu wa Nyongeza, hati yoyote itakayowasilishwa na Jumuiya ya Muungano wa Kikanda haitohesabiwa;

4. Kwa masuala yaliyomo ndani ya mamlaka zao, Jumuiya za Muungano wa Kikanda zinaweza kutumia haki yao ya kupiga kura katika mikutano ya Nchi zilizoridhia kwa idadi sawa ya kura na ile ya Nchi wanachama wao ambao zimeiridhia Mkataba huu wa Nyongeza. Hata hivyo, Jumuiya hizo hazitotumia haki ya kupiga kura ikiwa mmoja wa Nchi mwanachama wake ametumia haki yake ya kupiga kura, na kadhalika.

## Ibara ya 13

1. Kwa kutegemeana na ni lini Mkataba huu wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu utaanza kazi, Mkataba wa Nyongeza utaanza kutumika siku ya thelathini baada ya kuwasilishwa kwa hati ya kumi ya kuiridhia au kuikubali;

2. Baada ya kuwasilishwa kwa hati ya kumi na Nchi au Jumuiya ya Muungano wa Kikanda iliyoridhia, kuthibitisha rasmi au kuukubali Mkataba huu wa Nyongeza ndipo itakapoanza kutumika rasmi. Nchi husika itaanza kubanwa na Itifaki hii ya Hiari siku ya thelathini tangu ilipowasilisha hati yake kuridhia.

## Ibara ya 14

1. Shaka lolote linalopingana na lengo au makusudio ya Itifaki ya Hiari halitoruhusiwa.

2. Shaka linaweza kuondolewa wakati wowote.

## Ibara ya 15

1. Nchi yoyote iliyoridhia inaweza kushauri marekebisho ya Mkataba wa Nyongeza na kuyawasilisha kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Katibu Mkuu atawasilisha marekebisho yoyote yanayopendekezwa na Nchi

zilizoridhia pamoja na ombi la kuzitaka zimjulishe iwapo zinakubali kuitishwa kwa mkutano wa Nchi zilizoridhia kwa madhumuni ya kuzingatia na kufanya maamuzi juu ya mapendekezo yaliyowasilishwa. Itapotokea kwamba ndani ya miezi minne tokea tarehe ya mawasiliano hayo angalau theluthi moja ya Nchi zilizoridhia zimekubali kuitishwa mkutano, Katibu Mkuu ataitisha mkutano chini ya usimamizi wa Umoja wa Mataifa. Marekebisho yoyote yatakayopitishwa kwa wingi wa theluthi mbili ya kura za Nchi zilizohudhuria na kupinga kura, yatawasilishwa mbele ya Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa na Katibu Mkuu kwa kuidhinishwa na kisha kwa Nchi zote zilizoridhia ili yakubaliwe.

2. Marekebisho yaliyopitishwa na kuthibitishwa kwa mujibu wa aya ya 1 ya ibara hii, yataanza kutumika siku ya thelathini baada ya hati za kuyakubali zilizowasilishwa kufikia theluthi mbili ya Nchi zilizoridhia siku ya kupitishwa kwa marekebisho husika. Baadae marekebisho yataanza kutumika kwa Nchi yoyote siku ya thelathini kufuatia kuweka hati yake ya kuyakubali. Marekebisho hayo yatazibana zile Nchi zilizoridhia ambazo zimeyakubali.

## Ibara ya 16

Nchi iliyoridhia inaweza kujitoa katika utekelezaji wa Itifaki ya Hiari kwa kumpelekea Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa taarifa ya maandishi kuhusu kujitoa kwake. Kujitoa huko kutakuwa na nguvu mwaka mmoja baada ya tarehe ambayo Katibu Mkuu alipokea taarifa hiyo.

## Ibara ya 17

Mkataba wa Nyongeza utaweza kupatikana kwa njia ambayo watu wataipata kwa wepesi.

## Ibara ya 18

Nakala za Mkataba wa Nyongeza katika lugha za Kiarabu, Kichina, Kiingereza, Kifaransa, Kirusi na Kihispania zitakuwa sawa sawa na ni nakala rasmi.

**MBELE YA MASHAHIDI,** wanadiplomasia wenye dhamana za Serikali zetu, tumetia saini Mkataba huu wa Nyongeza.